



26/04/2022

TANGAZO LA MNADA WA KEMIKALI

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) itauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mapipa (170) yenye ujazo wa Lita 200 kila moja, ya kemikali aina ya Ethly Alcohol tarehe 10/05/2022 kuanzia saa nne 4.00 asubuhi kwenye Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kaskazini Arusha iliyoko Barabara ya Sekei Pemba jirani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

MASHARTI YA MNADA

1. Wadau wa kemikali waliosajiliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tu ndiyo watakaoruhusiwa kushiriki na kununua kemikali katika mnada.
2. Kila mdau wa kemikali atakayehudhuria mnada huu atatakiwa kuonesha cheti cha usajili "**Certificate of Registration**" kinachotolewa na Ofisi ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali kabla ya kuruhusiwa kushiriki mnada huo.
3. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia **ishirini na tano (25%)** ya thamani ya kemikali atakayonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya mnada kufanyika. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kemikali na amana iliyolipwa **haitarudishwa**.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua kemikali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia/ kukagua kemikali itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya kufanyika mnada husika kwa saa za kazi.
6. Mnada utanza saa Nne (04.00) asubuhi katika ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kanda ya kaskazini Arusha iliyoko Barabara ya Sekei Pemba jirani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Imetolewa na;

Sylvester Omary

**Msimamizi wa Kitengo Cha mawasiliano na Uhusiano
kwa Umma.**